KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 20, Issue 3
23rd Rabi uth-Thaani 1433
16th Mar, 2012

USOOL-UL-FIQH

Na: Shaykh 'Abdur-Rahmân ibn Nâsir as-Sa'dî (d. 1383 AH / n/a CE)

Kila sifa njema ni za Allaah. Tunamsifu Yeye kwa Majina Yake mazuri na Sifa bora alizonazo; na kwa Hukmu zake na Qadar zilizokusanya kila kitu katika ulimwengu huu; na Sheriya zake za kuhukumu zilizokusanya kila Nyanja za hukmu; na hukmu Zake kuhusiana na malipo mema kwa wenye kutenda mema, na adhabu kwa wenye kutenda maovu.

Nashuhudia yakwamba hapana anayestahiki kuabudiwa kwa kweli isipokuwa Allaah Peke yake. Asiyekuwa na mshirika katika majina Yake, Sifa wala Hukmu. Na nashuhudia yakwamba Muhammad ni Mtumwa wake na Mjumbe, aliyezifafanua hukmu na Sheriya, akayabainisha yaliyo halali na yaliyo haraam, na akayathibitisha misingi na akayaeleza kwa kina - mpaka Dini ikakamilika na akazithibitisha mpaka zikawa imara. Ewe Mola! Msifu na umfikilizie Baraka za amani Muhammad, na juu ya jamii yake, Maswahaba zake na wale waliowafuata wao, hususan Wanavyuoni.

Kwa utangulizi: Haya ni makala kwa mukhtasar kuhusu Usool-ul-Fiqh, yasiyokuwa na utata katika maneno yake, yaliyo wazi katika kufahamika kwake, na yenye faida katika kuzisoma hukmu zake kwa kila mwenye kuzingatia maana zake. Twamuomba Allaah awanufaishe wote wawili, muandishi na msomaji. Kwa hakika Yeye ni Mwenye Huruma zaidi.

MLANGO WA KWANZA:

Usool ul-Fiqh ni utaalamu wenye kuhusiana na ushahidi wenye kumuwezesha Mtu kufahamu mas'ala ya fiqh. Kwani fiqh imetokamana na emma (i) Masaa'il (mas'ala) yenye kuhusiana na hukmu inayotokana na mojawapo ya mambo matano, au (ii) Ni Dalaa'il (Dalili) inayotumika baada ya kuyakagua na kuyabainisha mas'ala hayo.

Kwahivyo fiqh, kwa hakika ni ilmu ya mas'ala yakiandamana na dalili. Na dalili zenyewe ni sampuli mbili:

Ushahidi wa kina unaokusanya kila hukmu - kuanzia mwanzo hadi mwisho wa fiqh - wa aina moja; kama tusemavyo: "al-amr lil-wujoob (amri ni ishara ya uwajibikaji)." Au: "an-nahee lit-tahreem (makatazo ni ishara ya Uharamu)." Na dalili nyengine mfano wa hizo. Kwahiyo hizi ni miongoni mwa sehemu ya usoolul-fiqh.

Dalili kwa uakmilifu zinataka zifahamike kwa muangaza wa ushahidi uliokamilika. Kwahiyo, ikiwa hayo yamepatikana, basi hukmu zinaweza kutatuliwa.

Kwahiyo, hukmu zinahitaji ushahidi wake ukamilike, na ushahidi wenyewe uliokamilika unahitaji dalili kwa kina.

Kwahivyo, kwa mpangilio huu, tunatambua mahitaji na umuhimu wa kujua mas'ala ya Usool ul-Fiqh, na kwamba inasaidia mno katika ufahamu wa fiqh yenyewe, na kwamba ni misingi ya kufikia hitimisho kutokana na ithbati iliyopo ya kufanya ijtihaad katika ahkaam (kutoa hukmu).

MLANGO WA PILI:

Hukmu zilizozungukwa na fiqh ni aina tano:-

WAAJIB: Jambo ambalo mwenye kulifanya hulipwa wema, haliyakuwa mwenye kuliwacha ataadhibiwa.

HARAAM: Hii ni kinyume cha jambo la wajibu.

MASNOON: Jambo ambalo mwenye kulifanya hulipwa wema, haliyakuwa asiyelifanya haadhibiwi.

MAKROOH: Hii ni kinyume cha mapendekezo.

MUBAAH: Hii ni iwapo yote mawili (kufanya jambo au kuwacha jambo) ni sawa.

Zile hukmu ambazo ni waajib zimegawanyika kwenye matapo mawili: fardh 'ayn (uwajibikaji wa kila mtu), kitendo kinachomuwajibikia kila mtu mukallaf (aliyekalifishwa na sheriya), baaligh (aliyebaleghe), 'aaqil (mwenye akili). Hukmu nyingi za kisheriya huingia kwenye orodha hii. Ya pili ni fardh kifaayah (uwajibikaji wa mkusanyiko), matendo yanayotekelezwa kutokamana na uwajibikaji wa umma, na wala sio kwa kila mtu makhsusi, kama vile kusoma vitagaa mbalimbali vya ilimu yenye manufaa na viwanda vyenye manufaa.; muadhini, kuamrisha mema na kukataza maovu, na mas'ala mengine kama hayo.

Hukmu hizi tano zimekhitilafiana kwa mapana kulingana na hali zake, daraja zake na athari zake.

Kwahiyo, jambo lolote lenye maslaha, basi Mpanga Sheriya (Allaah) huwa ameamrisha utekelezaji wake kwa emma uwajibu au ukokotezo. Lolote lenye (mafsadah) madhara, basi Mpanga Sheriya (Allaah) huwa amekataza utekelezwaji wake kwa emma kuharamisha moja kwa moja au amelifanya kuwa makruhu.

Kwahiyo asili hii imekusanya mas'ala yote yaliyoamrishwa au yaliyokatazwa na Muweka Sheriya. Amma kuhusu yale mas'ala ambayo Muweka Sheriya aliyoyahalalisha na kuyaruhusu, basi mara nyengine huwa yanaongoza katika kunako mazuri, na kwahivyo huunganishwa na mas'ala yaliyoamrishwa, na kwa mara nyengine hupelekea katika kunako mabaya na kwahivyo huunganishwa na mas'ala yaliyokatazwa. Kwahivyo hii ni asili kubwa ambayo: "al-wasaa'ilu lahaa ahkaamul-maqaasid (njia huchukuwa hukmu sawa na malengo yake)." kutokamana na haya tumeilimika yakwamba: "maa yatimmul -waajib illaa bihi fahuwa waajib (lolote linalohitajika kukamilisha lililo waajib, lenyewe huwa ni waajib)."

Vilevile, lolote linalohitajika kutekeleza

YALIYOMO
USOOL-UL-FIQH 1 - 3

jambo “masnoon” huwa lenyewe ni lenye kusisitizwa.
Lolote lenye kupelekea kwenye kufanya jambo la haraam, huwa lenyewe ni haraam. Na lolote lenye kupelekea kwenye jambo makruhu, huwa lenyewe ni Makrooh.

MLANGO WA TATU:

Adillah (Dalili) ambazo fiqh hutokamana nazo ni sampuli Nne:
Kitaab na Sunnah, na hii ndiyo misingi ambayo kwayo hawa Mukallafoon huzungumziwa, na ambayo juu yao ndipo ilipojengwa Dini yao. Kisha ‘Ijmaa’ na al-Qiyaas us-Swaheeh. Mawili haya yametokamana na Kitaab na Sunnah.
Kwahiyo fiqh, kwa ukamilifu wake - huwa haitoki nje ya mabano haya manne ya usool (misingi). Ahkaam nyingi zilizo muhimu zimeashiriwa na dalili (adillah) hizi Nne. Zimeashiriwa na nusoos kutoka kwenye Kitaab na Sunnah; na wanavyuoni wana ’Ijmaa’ kuhusiana nayo, nazo zimeashiriwa na “Qiyaas us-Swaheeh kwa sababu ya mambo yanayohitajika ya manufaa, ikiwa ilikuwa ni maamrisho; au mambo yenye madhara yaliyomo ndani yake, ikiwa ilikuwa ni mambo ya haraam. Hukmu chache sana zimekhalifiana baina ya wanavyuoni. Katika hali nkama hiyo, hukmu iliyo karibu sana na ukweli ni ile iliyofungamanishwa na hizi asli (usool) Nne.

MLANGO WA NNE:

KUHUSIANA NA KITAAB NA SUNNAH:
Ama kuhusu Kitaab: Basi ni Al-Qur’an ul -’Adheem, maneno ya Mola wa Walimwengu wote, kilichoteremshwa na Roho muaminifu juu ya Moyo wa Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ili apate kuwa ni muonyaji kwa walimwengu wote kwa ulimi ulio faswaha wa lugha ya kiarabu kuhusiana na yote waliyosimamia katika mahitaji yao katika kuwanufaisha wao katika Dini yao na Dunia yao. Kitaab cha Allaah ni kile kinachosomwa kwa ndimi, kikaandikwa kwenye miswahafu na kuhifadhiwa kwenye nyoyo kuhusiana na: “**Haitafikia batili mbele yake, wala nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye Hikima, ahimidiwaye.”** [Soorah Fussilat 41:42]
Amma kuhusu Sunnah: Ni maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), af’aal (vitendo vyake), na taqreer ya maneno ya vitendo vya wengineo.
Mara nyengine Ahkaamush-Shar’iyyah (hukmu za kisheriya) huchukuliwa kutoka katika maandiko maalum ya Kitaab na Sunnah; ikajulikana kama andiko lenye maana halisi, ikawa haina maana nyengine isipokuwa hiyo maana moja tu.
The ahkaamush-shar’iyyah. Mara nyengine huchukuliwa kutoka katika maana iliyo dhahiri inayofahamika kuwa ni yenye kuashiriya maana, kwa njia mbili za ujumla, ambazo ni kwa njia ya kimatamshi na kimaana. Mara nyengine huchukuliwa kutokamana na mantooq, inayosifiwa kuwa ni yenye kuashiriya hukmu kutokamana na maandiko ya Kitaab. Mara nyengine ahkaamush-Shar’iyyah huchukuliwa kutokamana na Mantooq: inayosifiwa kuwa ni kitu chenye kuashiriya hukmu inayotokamana na maandiko ya Kitaab. Mara nyengine ahkaamush-Shar’iyyah huchukuliwa kutokana na mafhoom: inayosifiwa kuwa ni kitu chenye ishara ya hukmu kutokamana na kuwepo kwa maafikiano ya maandiko, iwapo mafhoom itakuwa sawa na, au yenye nguvu kuliko mantooq. Au kwa maana iliyo na upana mkubwa iwapo mafhoom itakhalifiana na mantooq katika hukmu yake, haliyakuwa mantooq itakuwa imeunganishwa na wasf (sifa) au sharuti, katika kutokuwepo ambapo hukmu hutafautiana. Dalili katika Kitaab na Sunnah ni sampuli Tatu:
Dalaalah Mutaabiqah: Hapa ni pale tunapoweka neno kuashiriya maana zake zote.
Dalaalah Tadammun: Tunapotoa jina kuashiriya mojawapo ya maana zake.
Dalaalah Iltizaam: tunapoweka Neno kutoka kwenye Kitaab na Sunnah kuashiriya maana ambayo matokeo yake ni muhimu, na yenye kufuatilia katika ukamilishaji wake; na jambo lenye kuhukumiwa kwalo au lenye kupashwa habari zake, haliwezi kutokeza, isipokuwa kwa hilo.

MLANGO WA TANO:

Asili yenye kuhusiana na maamrisho katika Kitaab na Sunnah ni kwamba ni zenye kuashiriya mambo ya wajibu, isipokuwa iwapo kutakuwa na ushahidi kuashiriya kwake kuwa ni mustahabb (yenye kupendekezwa) au Mubaah (halali). Asili inayohusiana na makatazo ni kwamba ni zenye kuashiriya tahreem (uharamu), isipokuwa iwapo kutakuwa na ushahidi utakaoashiriya kuwa ni makrooh. Asili yenye kuyalinda maneno (kalaam) ni kwamba yanahitajika kuchukuliwa juu ya uhakika wake. Kwahiyo haifai kukimbiwa na kufuata majaaz - iwapo tutakubali hivyo, isipokuwa iwapo itakuwa ni vigumu kutumia kwa uhakika wake. Al-Haqaaiq ni sampuli tatu: (i) Shar’iyyah (iliyoelezwa kwa kutumia Sheriya), (ii) Lughawiyyah (iliyoelezwa kwa njia za lugha) na (iii) ‘Urfiyyah (inayoelezwa kwa njia za utamaduni).
Kwahiyo kila hukmu iliyoelezwa na Shaari’ (Allaah), basi ni waajib turudi kwenye maelezo ya kisheriya. Hatahivyo, aliyohukumu Muweka Sheriya (Allaah), ikawa hakutuchambulia, kutosheka na ufafanuzi wake wa ki-Lugha, basi ni waajib kurudi kwenye maana yake ya ki-Lugha. Lakini kwa lolote ambalo hatukubainishiwa kwa njia ya lugha au hata ya kisheriya, basi ni waajib kuirudisha kwenye desturi za watu na utamaduni wao. Muweka sheriya (Allaah) ana uwezo wa kubainisha kurudisha mas’ala haya kwa ’urf (matumizi ya ki-utamaduni), kama vile kuamrisha mema, kuishi kwa wema na mke na mas’ala mengine kama haya. Kwahiyo, zihifadhi usool hizi zinazohusiana na zile ambazo faqeeh anazozihitaji katika mahitaji yake yote ya fiqh.

MLANGO WA SITA:

Kutoka katika aya za Kitaab na Sunnah ni zile ambazo ni ‘aam (za ujumla), zinazoeleweka kama neno ambalo ni ajnaas, anwaa’ na afraad. Wingi wa matamshi kama haya ni sampuli hii. Matamshi mengine ni Khaas na huwa ni zenye kuashiria baadhi yake tu. Na lau kama hakupatikani ikhtilafu yoyote baina ya matamshi ‘aam na khaas, basi kila mojawapo hutendewa kazi kando. Hatahivyo, iwapo ikhtilafu itadhaniwa, basi ‘aam itakhusishwa na kuelezwa kwa undani na khaas. Kutoka katika maandiko, kunapatikana mutlaq na muqayyad. Imetiliwa mkazo kwa maelezo au mkazo wenye kutegemewa. Kwahiyo, mutlaq hutiliwa mkazo na kusahihishwa na muqayyad. Na katika maandiko kunapatikana mujmal na mubayyan. Hukmu nyingi katika Qur’an ni mujmal katika asili yake, lakini zikawa zimefafanuliwa waziwazi katika Sunnah. Kwahivyo ni wajibu kurudi kwenye Bayaan za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwani yeye ndiye mbainifu wa wazi kutoka kwa Allaah. Sawa na haya ni aya ambazo ni muhkam na zile ambazo ni mutashaabih. Ni wajibu kuzifahamu aya ambazo ni mutashaabih kwa muangaza wa aya ambazo ni muhkam.
Miongoni mwa aya ambazo ni naasikh na mansookh. Aya zilizofutwa katika Qur’an na Sunnah ni idadi chache. Kila panapopatikana uwezekano wa kuzipatanisha aya mbili, kwa uwezekano wa kila mojawapo kutendewa kazi kulingana na hali yake tafauti, basi itakuwa ni waajib kufanya

hivyo. Mtu hafai kuzitekeleza aya zilizofutwa, isipokuwa awe na aya kutoka kwa Muweka Sheriya (Allaah), au ikhtilafu iliyo dhahiri baina ya maandiko mawili yaliyo swaheeh ambapo hakupatikani uwezekano wa kusuluhisho kiasi cha kwamba kila andiko hutekelezwa kulingana na hali yake. Katika hali hii andiko lililokuja baadae hufuta la lililotangulia awali. Hatahivyo, ikiwa imeshindikana kutambua ni lipi andiko la awali na ni lipi la baadae, hapo ndipo tunapogeukia njia nyengine za tarjeeh (kufadhilisha andiko moja badala ya jengine). Kwa mfano, iwapo kutapatikana ikhtilafu iliyo dhahiri baina ya matamshi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kitendo chake, basi kipa-umbele hupewa katika matamshi yake. Hii ni kwa sababu matamshi yake, emma yanawakilisha amri au makatazo kwa umma wake, haliyakuwa vitendo vyake, katika hali hii ni, hufasiriwa kuwa ni jambo makhsusi kwake yeye peke yake. Kwahiyo zile khasaa'is (yenye kumuhusu Mtume (صلى الله عليه وسلم) peke yake) hutegemezwa juu ya asili yake. Vilevile, pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم) anapofanya jambo kama kitendo cha 'ibaadah, lakini asiamrishe utekelezaji wake, basi lililo sawa ni kwamba kitendo chake hiki ni ishara yakuwa ni mustahabb (lenye kupendekezwa). Iwapo atafanya jambo kama kitendo cha 'aadah, basi ni ishara yakwamba hilo ni mubaah (lenye kuruhusiwa). Lolote ambalo Mtume (صلى الله عليه وسلم) analoliruhusu katika matamshi na vitendo, basi hukmu ni miongoni mwa 'ibaadah (lenye kuruhusiwa), au vyenginevyo, kulingana na tabia ambayo ameruhusu matamshi kama hayo na vitendo.

MLANGO WA SABA:

Ama kuhusu ijmaa': ni makubaliano ya wanavyuoni wa Ijtihad juu ya hukmu mpya. Kwahiyo, kila tunapokuwa na yakini na ijmaa' yao, basi ni waajib kurudi nyuma na kuifuata, na hairuhusiwi kuipinga. Ni muhimu yakwamba kila ijmaa' ichukuliwe kutoka katika Kitaab na Sunnah. Ama kuhusu Qiyaas us-Swaheeh: huko ni kulinganisha tanzu la usaidizi na mzizi wake, kutokana na illah ya kawaida baina yao. Kwahiyo kila Mueka Sheriya (Allaah) anapoashiriya mas'ala, au akisifu kwa sifa fulani, au wanavyuoni wanapotoa uamuzi wao yakwamba hukmu imewekwa kwa sababu ya wasf, basi iwapo wasf huo khususan utapatikana kuwepo kwake katika mas'ala mengine, ambayo Allaah hakuyaekea hukmu yoyote makhsusi - pasi na kupatikana ikhtilafu baina yake na maandiko, basi ni waajib kuyashikanisha mambo hayo mawili kwenye hukmu yake. Hii ni kwa sababu Allaah hatafautishi baina ya mas'ala yenye kufanana kwenye tabia zake, kama ambavyo Yeye haunganishi baina ya mas'ala yasiofanana na yenye kupingana. Qiyaas hiki kilicho swaheeh ni al-Meezan kilichoteremshwa na Allaah. Na ndani yake muna uadilifu, na ni kwa hilo ambapo uadilifu hutambulika. Qiyaas huangaliwa na kuregelewa kama kutakosekana maandiko. Kwahiyo Asl hii huregelewa kwake iwapo hatopatikana asili nyengine. Na Qiyaas huunga mkono andiko ambalo Allaah alilolitolea hukmu, ndipo ikawa huafikiana na Qiyaas, na wala haipingani.

MLANGO WA NANE:

Wanavyuoni wa Usool wamefikia hitimisho kutokana na Kitaab na Sunnah katika Usool nyingi sana, ambapo walipojengea hukmu nyingi; ambapo walipofaidika nafsi zao na wengine. Miongoni mwa Usool zenyewe ni: "Al-yaqeen laa yazoolu bish-shakk [Al-Yaqeen haitanguki kwa shaka]." Chini ya msingi huu wameingiza 'ibaadat nyingi sana, mu'aamalaat, na huqooq. Kwahiyo yoyote atakaefurahia kwa kuwepo na shaka katika hayo, na arudi kwenye asl ya yaqeen. Vilevile wakafikia hitimisho: "al-aslut-tahaarah fee kulli shay [Msingi wa kila jambo ni twahara katika kila kitu]." Na : "al-aslul-ibaahah illaa ma dallad-daleelu 'alaa najaasatihi aw tahreemihi [Asl ni kuruhusiwa kutumia kila kitu isipokuwa iwapo kutakuwa na ushahidi wenye kuashiriya juu ya uchafu wake na uharamu]." Na : "al-aslul-ibaahah illaa ma dallad-daleelu 'alaa najaasatihi aw tahreemihi [Asl ni kuruhusiwa kutumia kila kitu, isipokuwa iwapo kutakuwa na dalili itakayoashiriya uharamu wake na uchafu wake]." Na: "al-aslul-ibaahah illaa ma dallad-daleelu 'alaa najaasatihi aw tahreemihi [Asl ni kuruhusiwa kutumia kila kitu isipokuwa iwapo kutakuwa na dalili itakayoashiriya uharamu wake na uchafu wake]." Na: "Asl ni kuwa huru na majukumu kuhusiana na uwajibikaji kwa viumbe, mpaka dalili ithubutu kinyume chake." Na: "Asl ni kuendelea kwa majukumu kuhusiana na uwajibikaji kwa Muumba, na kwa watumwa Wake, mpaka kupatikane ushahidi wa yakini wa kuwa huru na kutekeleza." Na kutokamana na hayo ni kwamba: "Al-mashaqah tajlibut-tayseer [Uzito huleta sahali]."

Juu ya misingi hii kunapatikana Rukhsa zote zinazokubalika kwenye misafara, na mambo ya 'ibaadaat, mu'aamalaat na mas'ala mengine. Na kutokana na hayo ni msemo wao: "Laa waajib ma'al-'ajaz wa laa muharram ma'ad-daroorah [hapana uwajibikaji pasi na kupatikana uwezo wa kutenda na wala hapana uharamu wowote pamoja na dharura]." Allaah hakutuwekea uwajibikaji kwa tusoyaweza kutenda kwa ukamilifu. Aliyotuwajibisha Allaah, kutokamana na mambo ya wajibu juu yetu, lakini akawa mja hana uwezo wa kuyatenda, basi uwajibikaji huo hutupiliwa mbali. Lakini hatahivyo, iwapo atakuwa na uwezo wa kutenda sehemu ya jambo hilo, atawajibika kulitenda kadiri ya uwezo wake, haliyakuwa ile sehemu asoiweza inatupiliwa mbali. Kuna mifano chungu nzima katika mas'ala haya. Vilevile, kila wanachohitaji viumbe, basi hakikufanywa kuwa ni haraam kwao. Ama kuhusu khabaaith, ambayo yaliyoharamishwa iwapo waja watakuwa na haja nayo kutokana na dharura, basi hapatokuwa na madhambi katika kuyatumia. Hii ni kwa sababu dharura huruhusu mambo yaliyo haraam tena yasiyobadilika. Na dharura hukisiwa kwa mahitaji yake, kwa ajili ya kupungusa madhara yake. Kwahiyo, dharura huruhusu matumizi ya mambo yaliyoharamishwa kwa kawaida kutokamana na vyakula, vinywaji, mavazi na mengine yasiyokuwa hayo. Na miongoni mwayo: "Al-umooru bi maqaasidiha [mambo huhukumiwa kutokana na sababu zake]." Yaingia katika fungu hili mambo ya 'ibaadaat na mu'aamalaat. Na miongoni mwayo: "Yukhtaaru 'alal-maslahatayn wa yartakab akhafal-mufsadatayn 'indat-tazaahum [kuchagua yaliyo bora baina ya maslaha sampuli mbili, au kuchagua madhara yaliyo machache baina ya madhara sampuli mbili]." Juu ya msingi huu mkubwa, mas'ala mengi yamejengewa hapo. Kwahiyo iwapo maslaha na hasara yanapatikana kwa vipimo sawa katika jambo fulani, basi: "dar'ul-mafaasid uwla min jalbil-masaalih [kuyaepuka madhara hupewa kipa-umbele kuliko kupata faida]." Na miongoni mwayo ni msingi: "Laa tutimmul-ahkaam illaa bi wujoodi shurootiha wa intifaa' mawaani'iha [Hukmu haitimii isipokuwa kwa kupatikana sharuti zake na makatazo ya vizuizi vyake]."

Huu ni msingi muhimu sana, uliojengewa kutokamana na mas'ala haya, hukmu na mambo mengine mengi. Kwahiyo kila kukipatikana shuruti za 'ibaadaat au

mu'aamalaat, au uthibitishaji wa haki utakosekana, basi hukmu hiyo haitokuwa sawa, na wala haitowezekana kuthibitishwa. Vilevile iwapo mawaani' (vizuizi) itapatikana, basi haitokuwa sawa, wala haitokuwa halali kisheriya. Shuroot za 'ibaadaat na mu'aamalaat ni: mas'ala yote ambayo ndani yake uhalali wa 'ibaadaat na mu'aamalaat unapatikana. Na shuroot hizi hujulikana kutokana na uta'alamu wa kina wa Sharee'ah. Kutokana na Asl hii, ma-Fuqahaa wameweza kuzibainisha faraaidh za 'ibaadaat mbalimbali na shuroot zake.

Ama kuhusu al-hasr: Ni kuthibitisha hukmu juu ya jambo fulani, haliyakuwa katika hali nyengine unaikataa. Kwa hilo, ma-Fuqahaa wameweza kubainisha shuroot za mambo mengi na mas'ala mengi, na mengine yasiyokuwa hayo, kisha hukmu isiwe ni yenye kuafikiana nayo. Na miongoni mwazo ni matamshi yao: "al-hukm yuduru ma'a 'illatihi thabootan wa 'adaman [Hukmu huzunguka kwenye illa yake katika zote mbili, uthibitishaji na ukanushaji]." Kwahiyo, ipatikanapo 'illatut-taamah (sababu ya illa kwa ukamilifu) - ijulikanayo yakwamba ina uhusiano na Sharee'ah, basi hukmu itapatikana; na ikosekanapo, basi hukmu haitoweza kuthibitishwa. Na miongoni mwazo ni msemo wao: "al-aslu fil-'ibaadaat al-hadhru illaa maa waradah 'anish-shaari' tashree'ahu, wal-aslu fil-'aadaat al-ibaahaa illaa maa waradah 'anish-shaari' tahreemahu [jambo la ki-msingi kuhusiana na matendo ya 'ibaadah ni Haraam. Isipokuwa yenye kuhusiana na Allaah kuhusiana na Sharee'ah, na msingi inayohusiana na mila na desturi ni Halaal, isipokuwa yenye kuhusiana na Allaah katika Sharee'ah kuhusiana na uharamu wake]."

Hii ni kwa sababu al-'ibaadah ni ile itokayo kwa Allaah, iwe ni kama uwajibikaji, au ukokotezo. Kwahiyo, chochote chenye kutoka katika mipaka hii haitozingatiwa kuwa ni kitendo cha 'ibaadah. Na kwa vile Allaah ametuumbia sisi kila kitu katika ardhi hii ili tupate kufaidika na kila kitu na kuweza kufanya matumizi yetu, isipokuwa yale ambayo Allaah ametuharamishia sisi.

Miongoni mwayo ni: "idhaa wajidat asbaabul-'ibaadaat wal-huqooq thabatat wa wajibat illaa idhaa qaaranahl-maani' [iwapo sababu za kufanya 'ibaadah zitakuwepo, zikawa zimethubutu na zikawa ni waajib, isipokuwa iwapo zitafungamanishwa na vizuizi]."

Na miongoni mwayo ni: "al-waajibaatu talzimul-mukallafeen [Uwajibikaji humlazimu mwenye kuwajibika ki-Sheriya]."

Kwahiyo takleef hufikiwa kwa: al-buloogh na al-'Aql. Hatahivyo, fidiya kutokana na madhara na kujeruhiwa inahitajika kutoka kwa mukallifeen na wengineo. Kwahiyo iwapo mtu ataingia kwenye umri wa kubaleghe na awe na akili timamu, basi zile hukmu wa uwajibikaji kwake zitatumika kwake. Na uwajibikaji makhsusi kutoka kwake vilevile utahitajika, maadamu atakuwa na sifa hizo zenye kuhitaji hayo. Wenye kusahau (naasee) na Wajinga (majaahil) hawatochukuliwa hatua kutokana na nukta ya maoni ya dhambi zao, wala nukta ya maoni ya fidiya ya jaraha au madhara.

MLANGO WA TISA:

Matamshi ya Swahaba mmoja - anaetambulika kama mtu yoyote aliyemuona Mtume (صلى الله عليه وسلم), akiwa amemuamini, na akafa na eemaan hiyo - na lau nitaenea na isipingwe, bali ikaafikiwa na Maswahaba, basi hiyo ni sampuli ya Ijmaa'. Na lau haijulikani kuwa ilisambaa, wala isijulikane kuwa palikuwa na lenye kulipinga hilo, basi kulingana na rai iliyo na usawa kiasi kikubwa, hiyo ni Hujjah (dalili). Hatahivyo, iwapo Maswahaba wengine walilipinga na wakalikhalifu, basi hiyo haitokuwa ni dalili.

MLANGO WA KUMI:

Amri ya jambo lolote, kinyume chake huwa haikosi uwezekano wa makatazo. Na ukatazo wa jambo lolote, kinyume chake huwa haikosi uwezekano wa maamrisho. Ukatazo wa jambo lolote hulazimisha yakwamba jambo hilo huwa halifai, isipokuwa iwapo kutakuwa na dalili inayoashiriya uhalali wake. Na amri yenye kuandama makatazo, huirudisha kwenye iliyolitangulia hilo. Na yote mawili, maamrisho na makatazo hulazimisha uwajibikaji wa haraka, lakini hazihitaji kurudia tena, isipokuwa iwapo itafungamanishwa na sababu maalum. Kwahiyo, inakuwa ni waajib au mustahabb kutekeleza kila sababu hiyo itakapokuwepo. Mas'ala ambayo ruhusa imetolewa ya chaguo ni sampuli nyingi. Kwahiyo iwapo chaguo lilitolewa kwa niya ya kumrahisishia mukallaf, basi chaguo hilo linapendekeza na kuchaguliwa. Iwapo chaguo limetolewa ili kupatikane maslaha fulani, basi kuchagua lile lenye faida kubwa ni waajib. Matamshi yenye kuashiriya ujumla ni: kull, jaami', al-mufridul-mudaaf, Nahyee, Nafee', istifhaam, au Shart (shuruti).

Na: "al-'ibrah bi 'umoomil-lafdh laa bi khusoosi-sabab [Somo lenyewe, au mazingatio ni kwenye ujumla wa neno, sio kwenye sababu yake makhsusi ya kisheriya]."

Jambo lililo khaass linaweza kumaanisha 'aam (kwa ujumla); na kinyume chake, maadamu kutakuwepo na qaraa'in (alama) zenye kuashiriya hayo. Khitaab (matangazo) ya Allaah kwa yoyote katika Ummah, au Matamshi yake katika mas'ala yoyote, kwa hakika yanamuhusisha kila mtu katika Ummah, na mas'ala yote makhsusi, isipokuwa iwapo kutakuwa na dalili inayoashiriya kuwa ni makhsusi.

Vilevile, msingi wa asili kuhusiana na vitendo vya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni kwamba Ummah wake umchukulie yeye kuwa ndiye kielelezo chao na mfano bora wa kufuatwa, isipokuwa iwapo kutapatikana dalili ya wazi yenye kuashiriya yakwamba jambo fulani ni makhsusi kwake yeye.

Ikiwa Allaah Atakataa kitendo cha 'ibaadah au mapatano ya ki-Jamii, basi hii ni ishara yakwamba jambo hilo halifai, au makatazo ya baadhi ya mas'ala yake muhimu. Hivyo basi, jambo hilo halitofanywa kuwa halifai kabisa kwa sababu ya makatazo ya baadhi ya mas'ala yaliyopendekezwa. Mikataba hutekelezwa au kufutwa kwa kila lenye kuashiriya haya, kutokana na yote mawili, matamshi na vitendo. Masaa'il ni sampuli mbili:

[i] Yale ambayo yaliyoafikiwa na wanavyuoni. Kwahiyo, hapa inatakiwa kuweka wazi na kuthibitisha dalili zilizo juu yake, kisha kuhukumu kulingana na usawa, baada ya kuweka wazi na kufikia hitimisho.

[ii] Yale ambayo Wanavyuoni waliyokhitilafiana. Kwahivyo, hapa inahitajika kuzijibu dalili za rai zenye kukhalifu. Hii ni haki ya Mujtahid (mwenye uwezo wa kufanya Ijtihaad) na mustadlil (mtekelezaji wa fikra kwa ujumla). Amma kumuhusu muqallid (mfuasi kwa njia za upofu), uwajibikaji wake ni kuwauliza watu wa 'Ilmu. Na taqleed ni: kuukubali msemo wa mtu, bila ya dalili. Kwahiyo mwenye uwezo wa utekelezaji wa fikra kwa ujumla, basi ni juu yake kufanya Ijitihaad na istidlaal, amma kwa asiyekuwa na uwezo, basi ni juu yake kufanya taqleed na aulize; kama ambavyo Allaah alivyoyataja mambo yote mawili katika Maneno yake: "Waulizeni watu wenye 'Ilmu ikiwa nyinyi hamujui." [al-Anbiyaa' 21:7].

Na Allaah Ndiye Mjuzi zaidi.

Twamuomba Allaah amfikilizie swala na salamu Mtume wake Muhammad (صلى الله عليه وسلم), na juu ya Ahli yake, Maswahaba zake na wafuasi wake.